**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE 21/12/2021**

**MHT.NA.1.TB/2021/2022/12/01. MAHUDHURIO.**

| | |
|---|---|
| 1. Shadrack W.Yomba | Mwenyekiti |
| 2. .Ndele Mwampamba | Katibu |
| 3. Sara Nalogwa | Mjumbe |
| 4. Osear Mwabusila | Mjumbe |
| 5. Rose Mikambi | Mjumbe |
| 6.Moses Mhagama | Mwanasheria |
| 7.Leonard Sunhwa | Sekretarieti |
| 8.George Semfuko | Sekretarieti |

**AGENDA MHT.NA.1. TB/2021/2022/12/02.**

1. Kufungua Kikao
2. Kusoma na kupitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha Bodi cha tarehe 24/08/2021
4. Yatokanayo na kikao chaBodi cha tarehe 24/08/2021
5. Kupita taarifa ya tathmini ya kuchanja mifugo dhidi ya mapele ngozi.
6. Kusoma na kupitia taarifa ya manunuzi ya robo ya kwanza 2021/2022.
7. Kupitia kablasha la zabuni ujenzi wa jengo la dharula pamoja na jengo la nyumba ya mtumishi zahanati ya Itengamatwi.
8. Kupitisha orodha ya wazabuni wa kufanya kazi na Halmashauri kwa mwaka wa Wa fedha 2021/2022.
9. Kujadili na kupitisha manunuzi mbalimbali na mpango wa manunuzi kama ifuatavyo;
   (i) Ujenzi wa wa kituo cha Afya Vumilia kwa njia ya Force Account kwa Tsh.250,000,000.00
   (ii) Ujenzi wa nyumba ya mtumishi zahanati ya Itegamatwi (three in one) kwa njia ya zabuni Tsh.90,000,000.00
   (iii) Ujenzi wa nyumba ya dharula hospitali ya Wilaya ya Urambo kwa njia ya zabuni Tsh.300,000,000.00
   (iv) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 58 Elimu Sekondari kwa nija ya Force Account Tsh.1,160,000,000.00
   (v) Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule shikizi vyumba 22 Elimu Msingi kwa nija ya Force Tsh.440,000,000.00 (Msumbiji-8,Chekeleni-2, Ichencha-2, Gimagi-2, Iyolelo-2, Maendeleo-2, Umoja B-2 na Mkanyageni-2.
   (vi) Ujenzi wa vyoo SWASH Shule za Katungulu, Kalembela, Sipungu, Ulasa jumla Tsh.126,045,502.24

19,800,000.00

10.Mengineyo.

11.Kufunga Kikao

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/03. KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti alifungua Kikao Saa 02:10 Asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao hicho cha kawaida na kuwasihi wachangie hoja ili kufanikisha kikao hicho kwa manufaa ya Halmasahuri.

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/04. KUSOMA NA KUPITISHA AGENDA**

Mwenyekiti alisoma agenda na wajumbe kupitia agenda moja baada ya nyingine na baaadaye wajumbe wakaridhia agenda zilizoletwa mbele ya kikao na kuweza kujadiliwa.

**AGENDA MHT.NA.1.TB/2021/2022/12/05.KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 24/08/2021**

Mwenyekiti aliwapitisha wajumbe muhtasari wa kikao cha tarehe 24/08/2021 baada ya hapo kwa ujumla wake kikao kiliuthibitisha muhtasari huo na kuruhusu usainiwe.

**AGENDA MHT.NA.1.TB/2021/2022/12/06. YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 24/08/2021.**

(i) Manunuzi yote yaliyoridhiwa yalifanyika kama ilivyopangwa ikiwa pamoja na

(a) Manunuzi ya dawa kwa Mshitili Chacha Magasi Pharmacy kwa gharama ya Tsh.7,464,320.00

(b) Manunuzi ya vifaa vya lishe Tsh.12,000,000.00

(c) Ununuzi wa huduma ya matengenezo ya mashine ya kufulia nguo Hospitali ya Wilaya ya Urambo Tsh.5,950,000.00 kutoka kwa mzabuni R-med tech & Consultancy.

(d) Ujenzi wa kutolea huduma za afya Tsh.267,414,610.00

(e) Kupitia taarifa ya timu ya tathmini kuhusu maombi ya wazabuni walioomba kuteuliwa kufanya kazi na Halmashauri ya Wilaya kwa mwaka 2021/2022.

(f) Ukamilishaji wa wodi ya wazazi na ukarabati wa jengo la Utawala Hospitali ya Wilaya Tsh.231,000,000.00.

(g) Upanuzi wa zahanati ya Songambele kuwa kituo cha afya kwa Tsh.400,000,000.00

(h) Ukamilishaji wa shule ya Unzali na Ugamba Tsh.7,300,000,00

(i) Ukarabati wa Urambo Motel Tsh.15,000,000.00

(j) Ukamilishaji wa shule ya msingi Juhudi Tsh.6,000,000.00

(k) Ukarabati wa zahanati ya Songambele Tsh.19,000,000.00

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/07.KUPITA TAARIFA YA TATHMINI YA KUCHANJA MIFUGO DHIDI YA MAPELE NGOZI.**

Bodi ya zabuni ilijadili taarifa ya PMU kuhusu taarifa ya tathmini ya uchanjaji wa mifugo dhidi ya mapele na kukubaliana kuwa Kampuni ya BACLEMA CO.LTD ya Shinyanga ipewe kazi hiyo kwa kuwa imekidhi vigezo vya kitathmini.
Pia wajumbe walishauri kampuni hii itoe taarifa kila wiki juu ya idadi ya ng'ombe waliochanjwa na kiasi cha fedha kilichopatikana na kulipa asilimia 10 ya Halmashauri.

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/08.KUSOMA NA KUPITIA TAARIFA YA MANUNUZI YA ROBO YA KWANZA 2021/2022.**

Bodi ya zabuni ilipitia taarifa ya manunuzi ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwa ni pamoja na manunuzi ya huduma,bidhaa pamoja na manunuzi kwa njia ya circular resolution.
Baada ya kupitia kwa kina bodi ya zabuni ilishauri taratibu za manunuzi ziendelee kuzingatiwa hasa urejeshaji wa masurufu ambao unaonekana kuwa ni changamoto kwa wengi.

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/09.KUPITIA KABLASHA LA ZABUNI UJENZI WA JENGO LA DHARULA HOSPITALI YA WILAYA YA URAMBO PAMOJA NA JENGO LA NYUMBA YA MTUMISHI ZAHANATI YA ITENGAMATWI.**

Mwenyekiti alimtaka katibu kutoa ufafanuzi kwa wajumbe kuhusu utaratibu na sheria inayowataka wajumbe wa bodi ya zabuni kushiriki kupitia na kufanya marekebisho pale inapobidi kuhusiana na kablasha za zabuni mbalimbali zinazoandaliwa na Halmashauri na kwa muda huu ilikuwa ni makablasha ya kazi ya ujenzi wa jengo la dharula pamoja na jengo la nyumba ya mtumishi zahanati ya Itegamatwi.
Baada ya kupitia kablasha hilo wajumbe wa bodi kwa pamoja waliridhia mchakato wa zabuni uendelee kwa kuwa limezingatia muongozo unaotolewa na mamlaka ya usimamizi wa manunuzi (PPRA).

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/010.KUPITISHA ORODHA YA WAZABUNI WA KUFANYA KAZI NA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**.

Bodi ya zabuni ilipitia na kujadili maombi ya wazabuni wawili walioomba kufanya biashara na Halmashauri baada ya kuwa wamekidhi viwango kama ifuatavyo.

(i) Ndagullah Eletronic and Water Supply kutoka Urambo.
(ii) Khalid Rwehumbiza muuzaji wa vifaa vya umeme kutoka Urambo.

Baada ya majadiliano na kwa umhimu wa vifaa vya umeme na upatikanaji wake bodi ya zabuni iliridhia maombi hayo ili kuongeza upatikanaji wa bidhaa za umeme na maji pamoja na kuongeza ushindani.

**AGENDA MHT.NA.1.TB/2022/12/11. KUJADILI NA KUPITISHA MANUNUZI MBALIMBALI NA MPANGO WA MANUNUZI KAMA IFUATAVYO;**

(i) Ujenzi wa wa kituo cha Afya Vumilia kwa njia ya Force Account kwa Tsh.250,000,000.00

(ii)Ujenzi wa nyumba ya mtumishi zahanati ya Itegamatwi (three in one) kwa njia ya zabuni Tsh.90,000,000.00

(iii) Ujenzi wa nyumba ya dharula hospitali ya Wilaya ya Urambo (EMD) kwa njia ya zabuni Tsh.300,000,000.00

(iv) Ujenzi wa vyumba vya madarasa 58 Elimu Sekondari kwa nija ya Force Account Tsh.1,160,000,000.00

(v) Ujenzi wa vyumba vya madarasa shule shikizi vyumba 22 Elimu Msingi kwa nija ya Force Account Tsh.440,000,000.00 (Msumbiji-8,Chekeleni-2, Ichencha-2, Gimagi-2, Iyolelo-2, Maendeleo-2, Umoja B-2 na Mkanyageni-2.

(vi) Ujenzi wa vyoo SWASH Shule za Katungulu ,Kalembela, Sipungu, Ulasa jumla Tsh.126,045,502.24

(vii) Ujenzi wa vyoo EP4R Shule za Mabatini, Urambo ,Izimbili Tsh. 19,800,000.00

Baada ya majadiliano ya Bodi ya zabuni kwa pamoja iliridhia manunuzi haya pamoja na maamuzi yote yaliyofanyika kwa njia ya circular resolution yaende kamati ya Fedha ,Uongozi na Mipango kwa hatua zaidi.

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/012. MENGINEYO.**

Hapakuwa na mengineyo

**AGENDA MHT.NA.1.TB /2021/2022/12/13. KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti alifunga Kikao mnamo saa 04:10 Asubuhi.

UMETHIBITISHWA

.................................... MWENYEKITI

.................................... KATIBU

TAREHE......06/04/2022